



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MADINI**



KITUO CHA JEMOLOJIA TANZANIA (TGC)

S.L.P. 119, Arusha. Barabara ya Mlima Themis-Njiro, Kiwanja Na 76-82,
Arusha Tanzania. **Nukushi** +255 272543241, **Simu: 0737816121**,
Barua pepe: tgc@madini.go.tz, **Tovuti:** www.tgc.ac.tz

NAFASI ZA MAFUNZO YA UONGEZAJI THAMANI MADINI

Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) ni Ktuo cha Serikali chini ya Wizara ya Madini, Kinatoa mafunzo na huduma mbalimbali katika fani za uongezaji thamani madini. Kituo kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa namba ya usajili REG/SAT/033

Kituo kinatangaza nafasi za mafunzo ngazi ya diploma na cheti katika fani za **ukataji na ung'arishaji madini ya vito (Lapidary)**; **Sayansi ya madini ya vito (Gemmology)**; na **usonara (jewellery design and jewellery manufacturing) mwaka wa masomo 2022/2023**, kama ifuatavyo:-

Na.	Aina ya kozi	Sifa za kujiunga	Muda	Muda wa kuanza
1.	Diploma katika teknolojia ya vito na usonara (Diploma in Gem and Jewellery Technology-NTA Level 4-6)	Muombaji awe na elimu ya kuanzia kidato cha nne na kuendelea, ufaulu wa kuanzia masomo manne (4) kwa Daraja D kidato cha nne	Miaka mitatu (3)	Septemba, 2022
2.	Ukataji, ung'arishaji na uchongaji madini ya vito na miamba (Gemstone cutting, polishing and carving - NVA-Level I-III). NB: Ngazi ya VETA	Muombaji awe na elimu ya kuanzia Darasa la saba na kuendelea	Miaka mitatu (3)	Septemba, 2022
3.	Usonara (Jewellery Design and Manufacturing)	Mtu yeyote mwenye nia ya kujifunza mbinu za uongezaji thamani madini	Miezi 6	Juni, 2022
			Miezi 3	Wiki ya kwanza kila mwezi
4.	Ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito (Lapidary)	Mtu yeyote mwenye nia ya kujifunza mbinu za uongezaji thamani madini	Miezi 6	Juni, 2022
			Miezi 3	Wiki ya kwanza kila mwezi
5.	Sayansi ya madini ya vito (Gemmology)	Mtu yeyote mwenye nia ya kujifunza mbinu za uongezaji thamani madini	Miezi 6	Juni, 2022
6.	Utambuzi wa madini ya vito (Gem Identification)	Mtu yeyote mwenye nia ya kujifunza utambuzi wa madini	Miezi 3	Wiki ya kwanza kila mwezi
7.	Utambuzi wa madini feki na madini ya vito yaliyo ongezewa thamani (Synthetic & treatment Gem Identification)	Mtu yeyote mwenye nia ya kujifunza utambuzi wa madini	Mwezi 1	Wiki ya kwanza kila mwezi
8.	Uthaminishaji wa madini ya vito (Coloured Gemstone Grading and Pricing)	Mtu yeyote mwenye nia ya kujifunza uthaminishaji wa madini ya vito	Mwezi 1	Wiki ya kwanza kila mwezi
9.	Uthaminishaji wa almasi (Diamond Grading and Pricing)	Mtu yeyote mwenye nia ya kujifunza uthaminishaji almasi	Mwezi 1	Wiki ya kwanza kila mwezi

NAMNA YA KUOMBA

- Muombaji ajaze fomu ya maombi akiambatisha nakala ya cheti cha kidato cha nne (form IV); Risiti ya malipo ya ada ya maombi (BPS); na kimojawapo kati ya cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha Taifa, Mpiga Kura, Leseni ya Udereva au Pasipoti ya Kusafiria.
- Muombaji atalipia ada ya maombi ya Tsh 10,000/= isiyorudishwa baada ya kupewa namba ya kumbukumbu ya malipo serikalini (Control Number) kutoka Kituoni atatakiwa kulipia tawi lolote la bank au wakala (NMB au CRDB).

Fomu zinapatikana katika Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) na Ofisi zote za Madini au tembelea tovuti za Kituo www.tgc.ac.tz au Wizara www.madini.go.tz.

Mwisho wa kupokea maombi ngazi ya diploma ni tarehe 15/08/ 2022.

NB: Wanawake watapewa kipaumbele zaidi, Kituo hakitoi ufadhili kwa wanafunzi watakaochaguliwa.

Kwa mawasiliano zaidi piga simu namba: **0737816121**, au tuandikie: tgc@madini.go.tz
Maombi pamoja na viambatanisho vitumwe kwenda kwa:-

**Mratibu,
Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC),
S.L.P. 119,
ARUSHA.**